

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA
MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A**

682



VITENDO VYA KUJIFUNZA HISABATI

Muda: Saa 3

Jumatano, 09 Mei 2018 asubuhi

Maelekezo

1. Karatasi hii ina sehemu A, B na C zenye jumla ya maswali **kumi na sita (16)**.
2. Jibu maswali **yote** katika sehemu A na maswali **mawili (2)** kutoka katika kila sehemu B na C.
3. Sehemu A ina alama **arobaini (40)** na sehemu B na C zina alama **thelathini (30)** kila moja.
4. Simu za mkononi na vitu vyote visivyoruhusiwa **havitakiwi** katika chumba cha mtihani.
5. Andika Namba yako ya **Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.



SEHEMU A (Alama 40)

Jibu maswali yote katika sehemu hii.

1. Taja hatua nne ambazo mwalimu anapaswa kuzingatia wakati anapomfundisha mtoto namna ya kuongeza vitu.
2. Hadithi ni mbinu mojawapo ya kufundishia dhana ya kuongeza na kupunguza vitu. Orodhesha sifa nne za hadithi bora.
3. Eleza kwa kifupi sababu nne za kutumia vihesabio wakati unapomfundisha mtoto vitendo vya kuhesabu vitu.
4. Taja mambo manne yanayomsaidia mtoto kutofautisha sarafu moja na nyingine wakati wa kujifunza fedha za Kitanzania.
5. Eleza kwa kifupi hatua nne za kuzingatia unapotaka kupima kitu.
6. Bainisha hatua nne utakazozipitia katika kumsaidia mtoto wa elimu ya awali kupunguza vihesabio vitatu kutoka kwenye vihesabio vitano.
7. Orodhesha mambo manne ambayo yanaweza kumsaidia mtoto kuchagua fedha wakati wa kulipia kitu dukani.
8. Taja mbinu nne za kukuza stadi za udadisi, ubunifu na ugunduzi katika kufanya vitendo vya Hisabati kwa mtoto wa elimu ya awali.
9. Taja aina nne za vipimo rasmi katika somo la Hisabati kwa kutoa mifano ya vizio vyake vya msingi.
10. Taja manufaa manne ya upimaji katika somo la vitendo vya kujifunza Hisabati.

SEHEMU B (Alama 30)

Jibu maswali mawili (2) kutoka katika sehemu hii.

11. Kuna mambo mbalimbali wanayofanya watu katika maisha ya kila siku yanayotambulisha nyakati za siku. Bainisha mambo matatu kwa kila nyakati za siku anazofundishwa mtoto wa elimu ya awali.
12. Kwa kutumia mbinu ya hadithi, eleza hatua nne utakazozitumia katika kufundisha utengenezaji wa mapambo.

13. Kwa nini mwalimu hushauriwa kutumia mbinu ya michezo zaidi katika kumfundisha mtoto wa elimu ya awali vitendo vya Hisabati? Toa hoja nne.

SEHEMU C (Alama 30)

Jibu maswali mawili (2) kutoka katika sehemu hii.

14. Eleza hatua nne utakazotumia katika kumfundisha mtoto wa elimu ya awali kuhesabu namba 1 hadi 5.
15. Fafanua misingi mitano ya ufundishaji na ujifunzaji wa vitendo vya kujifunza Hisabati.
16. Eleza vitendo utakavyofanya ili kumfundisha mtoto wa elimu ya awali dhana ya sifuri na kuiandika.